



TAARIFA KWA UMMA

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) inapenda kuufahamisha umma kuwa inapangisha majengo na maeneo ya wazi ndani ya uwanja wa Maonesho wa Mwl J.K Nyerere kwa ajili ya ofisi na huduma nyingine za kijamii wakati wa kipindi kisichokuwa cha Maonesho kinachoanzia tarehe 1 Agosti, 2018 hadi tarehe 31 Mei, 2019. Gharama za upangishaji wa majengo na maeneo hayo ni kwa mita za mraba (m²).

Wote mnakaribishwa kuja kuona majengo na maeneo yanayopangishwa wakati wa muda wa kazi kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 10.00 jioni.

Maombi ya upangishaji yatumwe kwa anwani ifuatayo:

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania,
S.L.P 5402,
DAR ES SALAAM
BaruaPepe: info@tantrade.go.tz
Simu: 0712 644410